

STEPS TOWARDS IMPLEMENTING THE TONGWE WEST DISTRICT AUTHORITY RESERVE FOR MPANDA DISTRICT COUNCIL

DISCLAIMER:

Any unintended errors in the translation of the title and abstract of this report are inadvertent and the responsibility of the ABCG Secretariat and do not necessarily reflect views of TNC, its partners or any persons cited in the study.

1. INTRODUCTION

The report of the Task Force to implement the process of establishing the Tongwe West District Authority Forest Reserve has six major components. These are: 1) Introduction, 2) objectives, 3) Implementation of the Goals, 4) geography and forest resources, 5) Challenges and recommendations, and 6) Conclusion. This task force was formed with a total of 17 people in order to meet the requirements of encompassing the relevant actors. The main purpose of this task force was to identify the boundaries of the forest reserves proposed to the District Council in a participatory manner. To fulfill this purpose, the task force had four main objectives.

The Task force had to successfully identify and verify the 24 GPS coordinate points that include stone beacons in the boundary between the forest and village authorities, and household boundaries between the region of Katavi and Kigoma. The revised villages include Lugonesi, Lwega, ivory, sisal, and Shamo Bugwe Settlement consisting of Bulamata and Chisenga. The wooded area has been determined to be 4,005km² and contains important natural resources like biodiversity, trees, water sources, mountains, and rivers. A total of 11 mountains, 10 water sources, 11 streams, 14 commercially value species, and the presence of 13 species of wildlife in the bush was confirmed.

In addition, the task force noted that many sources of head waters in the 18.52 km² village of Bugwe, which is expected to join with this forest will lead to comprehensive and sustainable conservation. This report presents the recommendations of the task force for the forest map in two approaches: 1) a map that is not inclusive of the Bugwe village and 2) a map which includes the village of Bugwe for the management decisions of the District Council. Despite the challenges and few drawbacks, their work has been accomplished much in planning the next step in making this forest reserve.





This report was made possible by the generous support of the American people through the United States Agency for International Development (USAID) under the terms of Cooperative Agreement No. RLA-A-00-07-00043-00. The contents are the responsibility of the Africa Biodiversity Collaborative Group (ABCG). Any opinions, findings, conclusions, or recommendations expressed in this publication are those of the authors and do not necessarily reflect the views of USAID or the United States Government. This publication was produced by **The Nature Conservancy** on behalf of ABCG.

HALMASHAURI YA WILAYA MPANDA



TAARIFA YA AWALI YA

MCHAKATO WA KUPANDISHA HADHI MSITU HURIA WA TONGWE MAGHARIBI KUWA MSITU WA HIFADHI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPANDA

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda
S. L. P. 1

MPANDA

Phone/Fax: 025 2820068

Email: halmashaurimpanda@iwayafrica.com. Website: www.mdc.go.tz

YALIYOMO

| | |
|--|-----------|
| ORODHA YA WASHIRIKI | 3 |
| 1. UTANGULIZI | 4 |
| 2. MALENGO MAKUU..... | 4 |
| 3. UTEKELEZAJI WA MALENGO MAKUU | 5 |
| 3.1 Kufanya makubaliano ya pamoja kati ya kikosi kazi (Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda) na vijiji vinavyopakana na msitu huria wa Tongwe Magharibi juu ya mipaka kati ya msitu wa hifadhi tarajiwa na mipaka ya vijiji iliyowekwa kisheria. | 5 |
| 3.1.1 Kijiji cha Lugonesi..... | 5 |
| 3.1.2 Kijiji cha Lwega:..... | 6 |
| 3.1.3 Kijiji cha Mpembe. | 6 |
| 3.1.4 Kijiji cha Vikonge..... | 6 |
| 3.1.5 Makazi ya Mishamo..... | 7 |
| 3.2. Kuweka alama na kunukuu nukta/pointi katika ardhi (coordinates) za mpaka kati ya msitu na kijiji kwa kutumia GPS | 7 |
| 3.2.1 Nukta za kuzunguka msitu na maelezo yake; | 7 |
| 3.2.2 Nukta za kuzunguka msitu na maelezo yake kwakujumuisha eneo Chepechepe la Bugwe (Bugwe water shade area)..... | 9 |
| 3.3 Kupata ramani na ukubwa wa msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda | 10 |
| 3.3.1 Ramani ya msitu kadiri ya nukta zilizopatikana katika soroveya bila kujumuisha eneo chepechepe la Bugwe;..... | 10 |
| 3.3.2 Ramani ya msitu kadiri ya nukta zilizopatikana katika soroveya kwa kujumuisha eneo chepechepe la Bugwe;..... | 10 |

| | |
|--|-----------|
| 3.3.3 Ramani ya Mkoa wa Katavi kuonyesha mahali msitu wa hifadhi tarajiwa ulipo kuhusianisha na tawala na maeneo mengine yaliyohifadhiwa;..... | 12 |
| 3.4. Kuandaa maelezo ya mipaka ya msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda | 14 |
| *3.5. Msitu wa Hifadhi Ukiunganishwa na eneo chepechepe la Kijiji cha Bugwe. | 15 |
| 4.0 JIOGRAFIA YA MSITU NA RASILIMALI ZILIZOMO. | 15 |
| 4.1 Mahali msitu ulipo..... | 15 |
| 4.2 Maumbile ya Msitu na Milima | 15 |
| 4.3 Rasilimali zilizomo ndani ya msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa..... | 15 |
| 4.3.1 Milima;..... | 15 |
| 4.3.2 Vyanzo vya maji | 15 |
| 4.3.3 Aina ya uoto na miti;..... | 16 |
| 4.3.4 Wanyamapori;..... | 16 |
| 5. CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO..... | 16 |
| 5.1 Changamoto; | 16 |
| 5.2 Mapendekezo; | 17 |
| 6. HITIMISHO | 18 |

ORODHA YA WASHIRIKI

| Na | JINA KAMILI LA MSHIRIKI | CHEO | FANI | KITUO CHA KAZI |
|----|----------------------------|-------------------------|-------------------------------------|----------------------------------|
| 1 | Nyambala, L. S. | Kiongozi Wa Timu | Mensuration & Managementi Ya Misitu | Halmashauri Ya Wilaya Ya Mpanda. |
| 2 | Demitrus Kamtoni | Katibu | Afisa Misitu/Sheria | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 3 | Ntengo, N | Nidhamu Na Mshauri Mkuu | Mpima | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 4 | Sokota, G A | Mshauri | Mhifadhi Wanyamapori | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 5 | Mackie Rojas | Mipango | Mtaalam Wa Ramani | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 6 | Gilbert Kasavila | Intelijensia | Mhifadhi Wanyamapori | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 7 | Eusebius Dachi | Mjumbe | Mhifadhi Wanyamapori | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 8 | Wenseslausi Kalimalwendo, | Mjumbe | Mhifadhi Wanyamapori | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 9 | Marko N. Masuba | Mzoefu Pori la Tongwe | Msaidizi Misitu | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 10 | Christopher Zacharia | Mzoefu Pori la Tongwe | Msaidizi Misitu | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 11 | L. Jovin, | Mwelekeo/Route | Gis Expert | Taasisi ya JGI |
| 12 | Japhet Kawimbe | Mjumbe | Sheria -Ardhi | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 13 | Betuel Mwandiga, | Mjumbe | Dreva | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 14 | M. Muksin, | Mjumbe | Dreva | Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. |
| 15 | Majaliwa Mambwe | Mjumbe | Kibarua | Mpanda mjini |
| 16 | Majaliwa Hatibu | Mjumbe | Kibarua | Vikonge |
| 17 | Alex Budegeye | Mjumbe | Kibarua | Sitalike |
| 18 | Norbet Jonh | Mjumbe | Kibarua | Ugalla |

1. UTANGULIZI

Taarifa ya Kikosi Kazi cha kutekeleza mchakato wa kuupandisha hadhi Msitu Huria wa Tongwe Magharibi ina vipengele vikuu sita. Vipengele hivyo ni 1) Utangulizi, 2) Malengo, 3) Utekelezaji wa Malengo, 4) Jiografia na rasilimali za msitu, 5) Changamoto na mapendekezo yake, na 6) Hitimisho. Kikosi kazi hiki kiliundwa na jumla ya watu 17 ili kukidhi mahitaji ya taaluma zinazohusika na dhumuni lake kuu. Dhumuni kuu la kikosi kazi hiki lilikuwa ni kubainisha mipaka ya msitu tarajiwa wa hifadhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kwa njia shirikishi. Ili kutimiza dhumuni hili kikosi kazi kilikuwa na malengo makuu manne.

Kikosi kazi kimefanikiwa kubaini na kuhakiki jumla ya nukta/points 24 zinazojumuisha nukta za GPS na mawe ya mipaka (beacons) katika mipaka kati ya msitu huo na mamlaka za vijiji, Makazi ya Mishamo au mpaka kati ya Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma. Vijiji vilivyopitiwa ni Lugonesi, Lwega, Mpembe, Vikonge, Bugwe na Makazi ya Mishamo yanayojumuisha Bulamata na Isenga. Eneo la msitu limebainika kuwa na ukubwa wa Km² 4,005 na linasheheni maliasili nyingi muhimu kama wanyama wa aina anuai, miti, vyanzo vya maji, milima, na mito. Jumla ya milima 11, vyanzo vya maji 10, mito 11, jamii 14 za miti ya thamani kibiashara, na aina 13 za wanyamapori ilithibitishwa kuwemo msituni humo.

Aidha, kikosi kazi hiki kilibaini kuwa vyanzo vingi vya maji vimo ndani ya kijiji cha Bugwe chenye ukubwa wa km² 18.52 ambalo kama litaunganishwa katika msitu huu tarajiwa itapelekea kuwa na uhifadhi kamilifu na endelevu. Katika taarifa hii, kikosi kazi kinawasilisha mapendekezo ya ramani za msitu huo katika mitazamo miwili; 1) ramani isiyojumuisha kijiji cha Bugwe na 2) ramani inayojumuisha kijiji cha Bugwe kwa maamuzi ya menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Pamoja na changamoto na vikwazo kadhaa, kazi hii imefanyika kwa ufanisi mkubwa ili kuandaa hatua zinazofuata katika kuufanya msitu huu kuwa wa hifadhi.

2. MALENGO MAKUU

Hatua hii ya kubainisha mipaka ilikuwa na malengo makuu yafuatayo;-

- 1) Kufanya makubaliano ya pamoja kati ya kikosi kazi (Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda) na vijiji vinavyopakana na msitu huria wa Tongwe Magharibi juu ya mipaka kati ya msitu wa hifadhi tarajiwa na mipaka ya vijiji iliyowekwa kisheria.
- 2) Kuweka alama na kunukuu nukta/pointi katika ardhi (coordinates) za mpaka kati ya msitu na kijiji/Makazi ya Mishamo

- 3) Kupata ramani ya msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na ukubwa wa msitu.
- 4) Kuandaa maelezo ya mipaka ya msitu tarajiwa wa hifadhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda

3. UTEKELEZAJI WA MALENGO MAKUU

3.1 Kufanya makubaliano ya pamoja kati ya kikosi kazi (Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda) na vijiji vinavyopakana na msitu huria wa Tongwe Magharibi juu ya mipaka kati ya msitu wa hifadhi tarajiwa na mipaka ya vijiji iliyowekwa kisheria.

3.1.1 Kijiji cha Lugonesi.

Zoezi la kubainisha mipaka ya msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kijijini Lugonesi lilianza tarehe 18/01/2013 kwa kukutana na uongozi wa kijijiji. Baada ya kurejea elimisho lililotolewa katika hatua ya uraghibishi uongozi wa kijiji ulitupatia watu watatu wanaojua mipaka ya kijiji hicho vizuri. Watu hawa ni ndugu Mathias Kabaje, ndugu George Sakamba na Robert Mlay.

Baada ya kupanga jinsi ya kuifanya kazi hiyo tukiwa katika moja ya madarasa ya shule ya msingi Lugonesi wawakilishi hao (akiwemo mwenyekiti wa Kijiji chao) walitueleza kuwa kijiji cha Lugonesi kinapakana na Makazi ya Mishamo kwa upande wa Kaskazini, Kusini kinapakana na kijiji cha Mwese, Mashariki kinapakana na kijiji cha Lwega. Wakati kwa Upannde wa Magharibi Kinapakana na Mkoa wa Kigoma.

Kazi ya kuzunguka mpaka katika maeneo ya kijiji hicho ilianza rasmi mnamo tarehe 20/01/2013. Kikosi kazi kilifika katika mto Lwegele uliopo umbali wa takribani kilometa 20 kaskazini mwa kijiji hicho ambao ndio mpaka wa kijiji cha Lugonesi kwa mujibu wa ramani **(Ramani Na 1, 2 na 3), cheti cha ardhi (Kiambatisho Na...) pamoja na fomu ya makubaliano ya mpaka huo kwa watu walioshiriki katika zoezi la upimaji wa mipaka ya kijiji hicho (Kiambatisho Na.....). Viambata hivyo vyote vimetokana na zoezi lililofanyika mwaka 2007.**

Aidha, wawakilishi hao walisema mpaka wa kijiji unatakiwa kuhamia katika mlima wa Mwikang'ombe uliopo zaidi ya kilometa 28 kutoka kwenye mpaka huo unaotambuliwa kisheria kwa sasa. Kutoka katikati ya kijiji hadi katika mlima huu kuna wastani wa takribani kilometa 37 kutoka katikati ya kijiji hicho cha Lugonesi. Walieleza kuwa wanataka msitu wa **Ntakata (Ramani Na 3)** uliosheheni aina lukuki za wanyamapori uwe ndani ya kijiji chao. Kufuatia matakwa hayo waliamrisha kikosi kazi hiki kutafuta mawe ya mpaka (beacons) na kwenda kuweka katika mlima wa Mwikang'ombe vinginevyo hawawezi kutupeleka huko ili kutuonyesha mahali wanapopendekeza kuwa mpaka wa kijiji cha Lugonesi.

3.1.2 Kijiji cha Lwega:

Katika mchakato wa kubaini na kuhakiki mipaka kati ya msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na mipaka ya kijiji cha Lwega, kikosi kazi kilifika kijijini Lwega tarehe 21/01/2013 uongozi ulitupatia watu watatu wenyeji wanaojua mipaka vizuri ya kijiji ambao ni Mzee Abdalah Juma, Mzee Mustapha Mohamed na Mzee Ally Katili.

Kama timu kwa pamoja tulitembelea pointi (beacons Na. VR 105) zinazotenganisha kijiji cha Lwega, Mpembe na msitu wa hifadhi tarajiwa. Pande zote ziliridhia kwa pamoja kuhusu mipaka hiyo na kuipongeza halmashauri kuhusu lengo hilo la kuhifadhi msitu huo pamoja na rasilimali zake ili ziweze kutumika kwa manufaa ya sasa na kizazi kijacho kwa faida ya vijiji vyote na wana Katavi kwa ujumla.

3.1.3 Kijiji cha Mpembe.

Katika kutekeleza malengo haya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, kikosi kazi cha watalaam kilifika kijiji cha Mpembe tarehe 22/01/2013 na kuungana na watu wawili wenyeji wanaoifahamu vyema mipaka ya kijiji hicho cha Mpembe. Wawakilishi hao wa kijiji ni Bwana Eliasi Rajabu na Musa Rajabu.

Maelezo ya wawakilishi hao wa kijiji kwa kuzingatia ramani ya kijiji chao walikubali na kuridhia mipaka hiyo kuwa ni mipaka halisi na sahihi. Pia walieleza kuwa kwa upande wa kaskazini kijiji chao kinapakana na kijiji cha Bugwe, kusini kinapakana na kijijini cha Katuma na Mashariki kuna kijiji cha Kasinde na Igalula. Pia, magharibi kuna kijiji cha Lwega na msitu tarajiwa.

Pia timu ya watalaam na wawakilishi wa kijiji cha Mpembe kwa pamoja tulifika katika mpaka wa kijiji (Jiwe Na NP 4) unaotenganisha vijiji cha Mpembe, Bugwe na msitu wa hifadhi tarajiwa wa halmashauri kwa ajili ya kuhakiki na kukubaliana. Kwa pamoja tulikubaliana bila tatizo.

3.1.4 Kijiji cha Vikonge.

Mchakato wa kubaini na kuhakiki mipaka kati ya msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na mipaka ya kijiji cha Vikonge, kikosi kazi kilifika kijijini Vikonge tarehe 24/01/2013 na kukutana na uongozi wa kijijini ambao walitupatia watu wawili ndugu Hatibu Rajabu na ndugu Alex John ambao ni wenyeji wanaoifahamu mipaka ya kijiji chao.

Baada ya kupanga jinsi ya kufikia maeneo yote yenye mawe ya mpaka kwa pamoja Kikosi kazi kiliongozana nao hadi mlima wa Mapalamanne ambao unatenganisha kijiji cha Vikonge, Makazi ya Mishamo, kijiji cha Bugwe na msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halmashauri ya Wilaya Mpanda (kwenye jiwe Na WAB 172 na VR 51). Wawakilishi hao wa kijiji walieleza kuwa kijiji cha Vikonge kinapakana na makazi ya Mishamo kwa upande wa kaskazini, wakati kusini kuna kijiji cha Majalila, Mashariki kuna msitu wa hifadhi na upande wa magharibi kuna kijiji cha Bugwe. Wote kwa kauli moja tulikubaliana na uhakiki ukakamilika.

3.1.5 Makazi ya Mishamo

Kikosi kazi kikiwa katika makazi ya Mishamo siku ya tarehe 26/01/2013 kilifanya maongezi ya awali na uongozi na kujipanga kwa kufanya kazi ya kubaini na kuhakiki mipaka hiyo siku inayofuata. Mkuu wa Makazi ya Mishamo (Bi Malietha Mallya-Msaidizi wa Mkuu wa Makazi ya Mishamo) na Harold Buhewa muangalizi wa ofisi ambao walikuwa ndio wenyeji wanaoifahamu mipaka hiyo kwa pamoja walitoa ushirikiano mkubwa na kufanya zoezi hili kuwa rahisi zaidi kuliko ilivyotarajiwa.

Pia Msaidizi wa Mkuu wa Makazi huyo alitueleza mipaka yake ya makazi sehemu inapopita kwa pande zote, pia alieleza kuwa kwa upande wa kaskazini wanapakana na msitu unaotarajiwa kutengwa, kusini wanapakana na msitu unaotarajiwa kutengwa, mashariki kuna hifadhi ya msitu wa Tongwe mashariki na magharibi kuna msitu unaotarajiwa kutengwa na kwa maana hiyo msitu unaotarajiwa kutengwa unazunguka zaidi ya robo-tatu ya eneo la makazi ya Mishamo .

3.2 Kuweka alama na kunukuu nukta/pointi katika ardhi (coordinates) za mpaka kati ya msitu na kijiji kwa kutumia GPS

3.2.1 Nukta za kuzunguka msitu na maelezo yake;

Uhakiki wa mipaka ulifanyika kwa kushirikisha vijiji vinavyopakana na eneo la msitu huo huria (General Land). Zoezi hili lilijikita katika kuwaelevesha wawakilishi wa pande mbili au tatu. Yaani kama kuna vijiji zaidi ya kimoja vinavyopakana na msitu huu basi pande tatu zilihusika ambazo ni wawakilishi wa vijiji hivyo na wawakilishi wa Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. Pale ambapo eneo hilo hupakana na kijiji kimoja tu basi pande mbili tu zilihusika ambazo ni wawakilishi wa kijiji husika na wawakilishi wa Halmashauri ya wilaya ya Mpanda. Pia baada ya kuelewa eneo linalohusika alama zinazo litambulisha eneo hilo ziliwekwa kwenye miti kwa kutumia rangi na hatimaye pointi/nukta za mahali lilipo jiwe la mpaka zilinukuliwa kwa kutumia kifaa kiitwacho GPS (Global Position System). Nukta zilizonukuliwa kwa kila eneo kuzunguka msitu huo huria zimewasilishwa katika jedwali Na 1a hapa chini.

Jedwali 1a: Kuonyesha nukta za mipaka ya msitu kadiri ya GPS

| Na | JINA LA KIJIKI/MAKAZI | NUKTA KATIKA ARDHI | | MAELEZO YA NUKTA HUSIKA (Attributes) |
|----|-----------------------|--------------------|-------------|---|
| | | 'Eastings' | 'Northings' | |
| 1 | Lugonesi | 194278 | 9320327 | Pointi hii ipo kwenye makutano ya mpaka wa kijiji cha Lugonesi na Mkoa wa Kigoma |
| | | 196503 | 9333362 | Pointi hii ipo kwenye makutano ya mpaka wa kijiji cha Lugonesi na Mkoa wa Kigoma |
| | | 232037 | 9307619 | Pointi hii ipo upande wa kaskazini magharibi wa kijiji cha Lugonesi kabla ya kuukuta mto Lwegele. |

| | | | | |
|----|--|--------|---------|---|
| 2 | Lwega | 223527 | 9330500 | Point hii ipo upande wa Kaskazini mwa kijiji cha Lwega ambapo mpaka wa kijiji unaungana na mto Lwegele |
| | | 231112 | 9308880 | Pointi hii ipo mita 20 kando ya barabara itokayo Mpanda kuelekea vijiji vya Lwega , Mwese na Lugonesi, pia ndilo jiwe linalotenganisha kijiji cha Lwega na Mpembe na msitu tarajia. |
| | | 236759 | 9326310 | Pointi hii ipo upande wa kaskazini magharibi wa kijiji cha Lugonesi kwa kuambaa na mto Lwegele ikitenganisha kijiji cha Lwega na Msitu tarajiwa wa Hifadhi. |
| *3 | Mpembe | 236729 | 9326179 | Pointi hii ipo katika jiwe linalotenganisha kijiji cha Mpembe , Bugwe na Msitu wa Hifadhi tarajiwea |
| 4 | Vikonge/Bugwe na Makazi ya Mishamo | 246557 | 9345644 | Pointi hii ipo juu ya mlima Maparamanne ambayo ni mpaka kati ya kijiji cha Bungwe/Vikonge na Makazi ya Wakimbizi ya Mishamo |
| 5 | Bugwe/Makazi ya Mishamo na Msitu wa Hifadhi tarajiwa | 246206 | 9344968 | Pointi hii ipo juu ya mlima Maparamanne mita 700 kusini magharibi ya pointi 240516/9345239 ambao ni mpaka kati ya Makazi ya Mishamo na msitu wa Hifadhi tarajiwa. |
| 6 | Mishamo | 194548 | 9370692 | Katika pointi hii mpaka unatokea mto Luguvu kuelekea kaskazini |
| | | 194548 | 9391651 | Katika pointi hii mpaka unakata kona kuelekea mashariki hadi unapokutana na mto Mlofwesi ambao pia ndio mpaka wa Msitu wa Hifadhi ya Tongwe (Tongwe FR). |
| 7 | Mto Mlofwesi | 242500 | 9391318 | Kutoka pointi hii mpaka unafuata mto Mlofwesi kuelekea Kaskazini |
| 8 | Tongwe | 240541 | 9418738 | Kutoka pointi hii mpaka unakwenda kusini mashariki hadi kwenye pointi 267227/9406742. |
| | | 267227 | 9406742 | Kutoka katika pointi hii mpaka unaelekea kusini magharibi zaidi hadi kwenye pointi 284610/9393277 unapoingia mto Malagalasi. |
| | | 284610 | 9393277 | Kutoka katika pointi hii mpaka unafuata mto Malagalasi hadi kwenye pointi 251069/9426083 ambapo ndipo unapoungana na mpaka kati ya mkoa wa Katavi na Kigoma. |
| 10 | Mpakani mwa Mkoa wa Katavi na Kigoma | 251069 | 9426083 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea magharibi hadi kwenye pointi 210707/9424006. |
| | | 210707 | 9424006 | Kutoka katika pointi hii mpaka unaelekea kusini magharibi hadi kwenye pointi 201141/9411959 |
| | | 201141 | 9411959 | Kutoka katika pointi hii mpaka unaelekea upande wa magharibi hadi kwenye pointi 158977/9409479 |
| | | 158977 | 9409479 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea kusini mashariki hadi kwenye pointi 178465/9394244 |
| | | 178465 | 9394244 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea kusini hadi pointi 194278/9320327 ambapo ndipo mpaka ulipoanzia katika kijiji cha Lugonesi. |

3.2.2 Nukta za kuzunguka msitu na maelezo yake kwakujumuisha eneo Chepechepe la Bugwe (Bugwe water shade area)

Aidha, kufuatia hali ya uwepo wa vyanzo vya maji vingi toka katika kijiji cha Bugwe ambavyo hutiririsha maji katika mito ya Katuma, Mnyamasi, Luguvu, Lugufu n.k kikosi kazi hiki kilizungukia maeneo ya kijiji hiki kwa upande wa Kaskazini, Mashariki na Kusini. Zoezi hili lilizaa nukta zilizomo katika **Jedwali Na 1b** kama linavyoonyeshwa hapa chini.

Jedwali 1b: Jedwali kuonyesha nukta za mipaka ya msitu kwa kujumuisha kijiji cha Bugwe

| Na | KIJIJI/M AKAZI | NUKTA ZA MIPAKA KATIKA ARDHI | | MAELEZO YA NUKTA HUSIKA (Attributes) |
|----|---|---------------------------------|-------------|---|
| | | 'Eastings' | 'Northings' | |
| 1 | Lugonesi | 194278 | 9320327 | Pointi hii ipo kwenye makutanio ya mpaka wa kijiji cha Lugonesi na Mkoa wa Kigoma |
| | | 196503 | 9333362 | Pointi hii ipo kwenye makutanio ya mpaka wa kijiji cha Lugonesi na Mkoa wa Kigoma |
| | | 232037 | 9307619 | Pointi hii ipo upande wa kaskazini magharibi wa kijiji cha Lugonesi kabla ya kuukuta mto Lwegele. |
| 2 | Lwega | 223527 | 9330500 | Point hii ipo upande wa Kaskazini mwa kijiji cha Lwega ambapo mpaka wa kijiji unaungana na mto Lwegele |
| | | 231112 | 9308880 | Pointi hii ipo mita 20 kando ya barabara itokayo Mpanda kuelekea vijiji vya Lwega , Mwese na Lugonesi, pia ndilo jiwe linalotenganisha kijiji cha Lwega na Mpembe na msitu tarajia. |
| | | 236759 | 9326310 | Pointi hii ipo upande wa kaskazini magharibi wa kijiji cha Lugonesi kwa kuambaa na mto Lwegele ikitenganisha kijiji cha Lwega na Msitu tarajiwa wa Hifadhi. |
| 3 | Mpembe | 236729 | 9326179 | Pointi hii ipo katika jiwe linalotenganisha kijiji cha Mpembe , Bugwe na Msitu wa Hifadhi tarajiwea |
| 4 | Bugwe | 236730 | 9326179 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea mashariki hadi mlima Mwenda Hill kwenye pointi 256520/9320476. |
| | | *256520 | 9320476 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea mashariki hadi pointi 262756/9320192 |
| | | *262756 | 9320192 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea kaskazini hadi pointi 261622/9337199 |
| | | * 261622 | 9337199 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea kaskazini magharibi hadi kwenye pointi 246557/9345644 |
| 5 | Vikonge/B ugwe na Makazi ya Mishamo | 246549 | 9345634 | Pointi hii ipo juu ya mlima Maparamanne ambayo ni mpa kati ya kijiji cha Bungwe/Vikonge na Makazi ya Wakimbizi ya Mishamo |
| 6 | Bungwe/M akazi ya Mishamo na Msitu wa Hifadhi tarajiwa | 246206 | 9344968 | Pointi hii ipo juu ya mlima Maparamanne mita 700 kusini magharibi ya pointi 240516/ 9345239 ambao ni mpaka kati ya Makazi ya Mishamo na msitu wa Hifadhi tarajiwa. |
| 7 | Mishamo | 194548 | 9370692 | Katika pointi hii mpaka unatokea mto Luguvu kuelekea kaskazini |

| | | | | |
|----|--------------------------------------|--------|---------|---|
| | | 194548 | 9391651 | Katika pointi hii mpaka unakata kona kuelekea mashariki hadi unapokutana na mto Mlofwesi ambao pia ndio mpaka wa Msitu wa Hifadhi ya Tongwe (Tongwe FR). |
| 8 | Mto Mlofwesi | 242500 | 9391318 | Kutoka pointi hii mpaka unafuata mto Mlofwesi kuelekea Kaskazini |
| 9 | Tongwe | 240541 | 9418738 | Kutoka pointi hii mpaka unakwenda kusini mashariki hadi kwenye pointi 267227/9406742. |
| | | 267227 | 9406742 | Kutoka katika pointi hii mpaka unaelekea kusini magharibi zaidi hadi kwenye pointi 284610/9393277 unapoingia mto Malagalasi. |
| | | 284610 | 9393277 | Kutoka katika pointi hii mpaka unafuata mto Malagalasi hadi kwenye pointi 251069/9426083 ambapo nipo unapoungana na mpaka kati ya mkoa wa Katavi na Kigoma. |
| 10 | Mpakani mwa Mkoa wa Katavi na Kigoma | 251069 | 9426083 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea magharibi hadi kwenye pointi 210707/9424006. |
| | | 210707 | 9424006 | Kutoka katika pointi hii mpaka unaelekea kusini magharibi hadi kwenye pointi 201141/9411959 |
| | | 201141 | 9411959 | Kutoka katika pointi hii mpaka unaelekea upande wa magharibi hadi kwenye pointi 158977/9409479 |
| | | 158977 | 9409479 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea kusini mashariki hadi kwenye pointi 178465/9394244 |
| | | 178465 | 9394244 | Kutoka pointi hii mpaka unaelekea kusini hadi pointi 194278/9320327 ambapo ndipo mpaka ulipoanzia katika kijiji cha Lugonesi. |


3.3 Kupata ramani na ukubwa wa msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halamshauri ya Wilaya ya Mpanda

3.3.1 Ramani ya msitu kadiri ya nukta zilizopatikana katika soroveya bila kujumuisha eneo chepechepe la Bugwe;


Zoezi la kuzunguka msitu huu lilifanikiwa na kutupatia ramani inayoonekana katika **Ramani Na 1** ikionyesha eneo hilo kama linavyobainishwa kwa rangi ya zambarawe. Eneo hili lina ukubwa wa kilometa za mraba 4,005 (Km²) na halijahusisha eneo lolote la ardhi ya kijiji wala Makazi ya Mishamo.

3.3.2 Ramani ya msitu kadiri ya nukta zilizopatikana katika soroveya kwa kujumuisha eneo chepechepe la Bugwe;

Baada ya kuzunguka eneo la msitu huu huria na kuchukua nukta (Points/coordinates) katika kila kona ilipatikana ramani inayoonekana katika **Ramani Na 2**. Katika ramani hii eneo hilo limebainishwa kwa rangi ya kijani kibichi. Endapo msitu huu utajumuisha eneo chepechepe la kijiji cha Bugwe kwa ujumla msitu huu utakuwa na ukubwa wa **4,441** km² bila kujumuihusisha eneo lolote la ardhi ya kijiji wala Makazi ya Mishamo ukiachia mbali kijiji cha Bugwe.




Ramani Na 1: Ramani kuonyesha mapendekezo ya eneo la msitu litakalohifadhiwa kuwa msitu wa hifadhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda.



Ramani Na 2: Ramani kuonyesha mapendekezo ya eneo la msitu litakalohifadhiwa ikijumuisha eneo chepechepe la kijiji cha Bugwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda

3.3.3 Ramani ya Mkoa wa Katavi kuonyesha mahali msitu hifadhi tarajiwa ulipo kuhusianisha na tawala na maeneo yaliyohifadhiwa;

Mkoa wa Katavi unamaeneo makubwa yaliyohifadhiwa ambayo ni misitu tisa ya hifadhi (2,801,168.6 ha), Hifadhi ya Taifa ya Katavi na maeneo makubwa ya wazi ambayo mojawapo ndilo linalopendekezwa katika taarifa hii kuwa msitu wa hifadhi. Pamoja na misitu ya hifadhi kuwa tisa (9) mkoani hapa, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda baada ya kugawanyika katika Wilaya mbili zinazo fanya jumla ya halmashauri nne: imebakiwa na misitu miwili tu ambayo ni midogo kwa ukubwa. Misitu hiyo ni msitu wa Hifadhi ya Nkamba na Msitu wa Hifadhi ya Tongwe East (**Angalia Ramani Na 3**).



Ramani Na 3: Ramani ya Mkoa wa Katavi kuonyesha msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa kwa kuondoa kijiji cha Bugwe

3.4 Kuandaa maelezo ya mipaka ya msitu wa hifadhi tarajiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda

Msitu wa Hifadhi tarajiwa ya ‘**Tongwe West Forest Reserve**’ imo ndani ya mipaka ya Mkoa wa Katavi. Msitu huu unapatikana kaskazini Magharibi ya Mkoa wa Katavi katika Wilaya ya Mpanda, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Mipaka ya msitu huu itakuwa kama ifuatavyo:

Upande wa Kusini;

Mpaka wa Msitu unaanzia kwenye jiwe namba **1 (RV 46)** lililopo katika makutanio ya mpaka wa kijiji cha Lugonesi na Mkoa wa Kigoma, ambao ni mpaka kati ya Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma. Kutokea jiwe namba **1** mpaka unaelekea Kaskazini Magharibi umbali wa kilometa 5.55 hadi jiwe namba **2 (RV 14)**, kutoka kwenye jiwe hili mpaka unaelekea Kaskazini Magharibi zaidi umbali wa kilometa 5.50 hadi jiwe namba **3 (NP_a)** ambapo mpaka unakutana na *Mto Lwegele*. Kutoka kwenye jiwe namba **3 (NP_a)** mpaka unaanza kufuata *Mto Lwegele* kuelekea Kusini Mashariki umbali wa kilometa 25.3 hadi kwenye jiwe namba **4 (VR 105 – 232037/9307619)** ambalo liko mita 25 kaskazini mwa barabara itokayo Mwese kuelekea Kijiji cha Lwega. Kutoka jiwe namba **4 (VR 105)** mpaka unaelekea kaskazini Mashariki hadi jiwe namba **5 (NP₄ - nukta 236759/ 9326310)** lililopo umbali wa kilometa 19.23 na ambalo linatenganisha kijiji cha Mpembe, Bugwe na msitu wa hifadhi tarajiwa.

Upande wa Mashariki;

Kutoka jiwe namba **5 (NP₄)** mpaka unaelekea upande wa Kaskazini mashariki kwa umbali wa kilometa 21.6 hadi jiwe namba **6 (WAB 172 – 246549/9345634)** juu ya Mlima wa Mapalamanne ambao ni mpaka wa kijiji cha Vikonge, Bugwe na Makazi ya Mishamo, kilometa 0.7 toka jiwe namba **6 (WAB 172)** mpaka unaelekea Magharibi hadi jiwe namba **7 (NP_b)** katika mlima huohuo wa Mapalamanne ndipo palipo na mpaka wa kijiji cha Bugwe, Makazi ya Mishamo na Msitu wa hifadhi tarajiwa. Kutoka jiwe namba **7 (NP_b)** mpaka unafuata *Mto Luguvu* kuelekea upande wa Kaskazini magharibi (umbali wa kilometa 52.8) hadi jiwe namba **8 (NP_c)**. Kutoka jiwe namba **8 (NP_c)** mpaka sasa unaelekea kaskazi umbali wa kilometa 21.1 hadi jiwe namba **9 (NP_d)**. Kutoka jiwe namba **9 (NP_d)** mpaka unaelekea upande wa Mashariki hadi jiwe namba **10 (NP_e)** lililoko umbali wa kilometa 47.7 ambapo mpaka wa msitu wa hifadhi tarajiwa unaungana na Msitu wa hifadhi wa Tongwe kwenye *Mto Mlofesi*. Kutoka jiwe namba **10 (NP_e)** mpaka unafuata *Mto Mlofesi* kuelekea Kaskazini hadi jiwe namba **11**, umbali wa kilometa 27.15. Kutoka jiwe namba **11** mpaka unaelekea upande wa kusini Mashariki kufuata mpaka wa msitu wa hifadhi ya Tongwe East umbali wa kilometa 29.76 hadi jiwe namba **12**. Kwa kufuata mpaka wa msitu wa hifadhi ya Tongwe East kutoka jiwe namba **12** umbali wa kilometa 21.85 mpaka unaelekea Kusini mashariki zaidi hadi jiwe namba **13** ambapo mpaka unapokutana na *Mto Malagalasi*.

Upande wa Kaskazini na Magharibi;

Kwa upande wa Kaskazini msitu huu unapakana na Mkoa wa Kigoma, hivyo, kutoka jiwe namba **12** mpaka unafuata mpaka mati ya Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katavi kwa pande zote za kaskazini na Magharibi hadi unapolikuta jiwe namba 1 ulipoanzia.

***3.5. Msitu wa Hifadhi Ukiunganishwa na eneo chepechepe la Kijiji cha Bugwe.**

Kutoka jiwe namba **6 (WAB 172)** mpaka unaelekea Kusini mashariki umbali wa kilometa 20.53 hadi mlima Mwenda Hill palipo na jiwe namba **7'**, kutoka mlima Mwenda Hill katika jiwe namba **7'** mpaka unaelekea Mashariki zaidi umbali wa kilometa 6.60 hadi jiwe namba **8'** linalotenganisha vijiji vya Igalula, Majalila na Vikonge, kutoka jiwe namba **8** mpaka unaelekea Kaskazini umbali wa kilometa 16.56 hadi jiwe namba **9'**, Kutoka jiwe namba **9'** mpaka unaelekea Kaskazini Magharibi umbali wa kilometa 16.67 hadi mlima Mapalamanne unapounganisha kwenye jiwe namba **7** linalotenganisha kati ya kijiji cha Bugwe na Vikonge.

4.0 JIOGRAFIA YA MSITU NA RASILIMALI ZILIZOMO.

4.1 Mahali msitu ulipo.

Msitu huu uliotengwa kwa matarajio ya kuhifadhiwa kuwa msitu wa hifadhi uko upande wa Kaskazini Magharibi mwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Kwa upande wa Kaskazini msitu huu unapakana na wilaya ya Uvinza iliyoko mkoani Kigoma. Upande wa kusini msitu huu unapakana na vijiji vya Lugonesi na Lwega. Upande wa Mashariki msitu huu unapakana na vijiji vya Mpembe na Vikonge wakati upande wa magaribi msitu huu utapakana na Mkoa wa Kigoma. Makazi ya Mishamo yanazungukwa na msitu huu kwa pande zote isipokuwa upande wa Mashariki.

4.2 Maumbile ya Msitu na Milima

Msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa una sura ya milima na mabonde yenye mchanganyiko wa mawe, miti, ardhi oevu/chepehepe na nyasi . Pia vipo vyanzo vya maji na mito mikubwa na yenye kutililisha maji mwaka mzima na mito mingi midogomidogo ya msimu na ya kudumu.

4.3 Rasilimali zilizomo ndani ya msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa

4.3.1 Milima;

Msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa una milima mingi ikiwemo ifuatayo; mlima Mwikang'ombe, mlima Mapalamanne, mlima Mkudusi, mlima Kasitunda, mlima Mwenda Hill, mlima Ikale, mlima Kasilungu, mlima Kashenene, mlima Kasimu, mlima Sitebhesyambemba na mlima Mpasijasilungwe.

4.3.2 Vyanzo vya maji

Eneo hili la msitu ni tunu ya pekee katika Mkoa wa Katavi kwa sababu imesheheni vyanzo vya maji visivyopungua kumi (10). Vyanzo hivyo ni pamoja na vile vinavyo zaa mto Katuma, mto Bugwe, mto Luguvu, mto Lwegele, mto Mfilisi, mto Mlofwesi, mto Mnyamasi, mto Lugufu, mto Lugonesi, mto Pacha, mto Sabaga, na mingine mingi. Upekee wa msitu huu kwa wana Katavi ni kwamba vyanzo vya maji hutiririsha maji yake kwa wakazi wa

Mkoa huu tofauti na mito inayoanzia katika misitu kama Msitu wa Hifadhi wa Milima ya Mulele, Inyonga, North-east Mpanda ambayo maji yake hutiririka na kuhudumia watu walio nje ya mkoa huu wa Katavi kupitia Mfumo Ekolojia wa Ugalla (Ugalla ecosystem), Malagalasi-Muyovozi Wetlands hadi mfumo wa Ziwa Tanganyika (Lake Tanganyika System).

4.3.3 Aina ya Uoto na miti;

Aina ya uoto unaopatikana katika msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa ni “Miombo woodland”. Hii ni miombo ya uwanda wa chini (Low land Miombo woodland). Aidha, msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa kama ilivyo misitu mingine ya Ki-Ikweta inajumuisha aina nyingi za miti (Tree species) takribani aina 120 za miti. Hata hivyo, miti iliyotawala eneo hili ni pamoja na Mninga, Mkongo, Mkurungu, Mpilipili, Mtundu, Miyombo, Masaka, Mbanga, Mkusu, Mfuru, Msofu, Mkuni, Mgando na Mingineyo Mingi.

4.3.4 Wanyamapori;

Wanyamapori wanaopatikana kwa wingi katika msitu unaotarajiwa kuhifadhiwa ni Nyati, Tembo, Pofu, Mbega wekundu na weupe, Simba, Kongoni, Swala, Palahala, Nguruwe pori, Sokwe, Pongo, kima, Nyani, Tumbili, aina mbalimbali za nyoka na ndege wa aina mbalimbali. Wanyamapori wengi wanapatikana sehemu za mabondeni, milimani na nyikani. Lakini makundi makubwa ya wanyama hawa wamerundikana katika msitu uitwao “**Ntakata**” na kuwavutia watu wengi kuwahodhi kwa manufaa binafsi/ya wachache.

5. CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO

5.1 Changamoto;

- I. Mazingira ya kazi hii yalikuwa magumu kutokana na kazi kufanyika kipindi cha masika hivyo kufanya baadhi ya maeneo kutokufikika kiurahisi kutokana na mito mingi kujaa maji.
- II. Kutokuwa na fedha za dharula zilizotengwa rasmi kwaajili ya matengenezo ya dharula ya magari yanayotumika katika kazi hii inayoendelea na kusababisha isimame kusubiri matengenezo madogomadogo ya magari hayo (STK 4227 na SM 4133).
- III. Baadhi ya vijiji kutokuwa na uongozi kama kuwa na makaimu watendaji wa vijiji waliopewa madaraka kienyeji bila ofisi ya DED kufahamu mfano (Bulamata) na kutokuwepo kabisa kwa uongozi wa vijiji kama Vikonge ambapo kiongozi mmoja anahodhi maamuzi ya kiuongozi (**Rejea Kiambata Na A**).
- IV. Bulamata na Isenga ambayo katika mpango kazi (**Plan A**) tulitambua kama vijiji mamlaka za maeneo hayo zimekanusha kuwa si vijiji. Hivyo kushindwa kufanya taratibu za kubainisha mipaka kwa mfumo shirikishi.

- V. Uchache na uchakavu wa Mahema kwa ajili ya kuweka kambi msituni ni changamoto mojawapo, watumishi wamekua wakisongamana ndani ya hema moja na hata kuvujiwa na maji wakati mvua inanyesha.
- VI. Ukosefu wa vyombo vya kupikia na kulia chakula wakati wa tukiwa kambini.
- VII. Kutokuwepo na vifaa muhimu vya kupigia kambi kama vile Sanduku la huduma ya kwanza na ‘Sleeping bag’ ambazo ni muhimu sana kutokana na hali ya baridi kali kwa Misitu ya milimani.

5.2 Mapendekezo;

1. Kazi hii ilipangwa kufanyika kuanzia Septemba 2012 hadi Novemba 2012 lakini ilishindikana kutokana na kuchelewa kwa taratibu za kifedha. Ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi kama hizi zilizo na vikwazo vya majira ya mwaka, inafaa mpango kazi unaowasilishwa kwa uongozi ufuatwe ili kuepusha kazi hizo kuahirishwa hadi msimu usiotarajiwa kama msimu wa mvua.
2. Kutokuwa na fedha za dharula zilizotengwa rasmi kwaajili ya matengenezo ya dharula ya magari yanayotumika katika kazi hii inayoendelea na kusababisha isimame kusubiri matengenezo madogomadogo ya magari hayo (STK 4227 na SM 4133).
3. Ofisi ya Mkurugenzi ifanye taratibu za kuunda uongozi kijiji cha Vikonge. Pia DED apeleke watendaji wa vijiji wenye sifa stahiki katika vijiji vya Bulamata na Vikonge.
4. Suala la Bulamata na Isenga kutotambulika kama vijiji vya watanzania litazamwe upya ki diplomasia kwani pana uongozi tu lakini hawana milki.
5. Halmashauri kwa kutumia fedha za uwindishaji wa kitalii na asilimia 25% ya leseni za uvunaji mazao ya misitu iweke mpango wa makusudi wa kununua vifaa vya kazi za doria katika mapori.
6. Tunapendekeza kuwa msitu huu uhifadhiwe chini ya umiliki wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na kwamba mfumo wa usimamizi ujikite katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu(PFM) ambapo kijiji au muungano wa vijiji unaweza kuomba kuusimamia msitu wote ama sehemu ya msitu huo kwa ubia (JFM) na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Pia kwa kanda iliyo na wanyamapori vitalu/kitalu cha uwindishaji ki/vinaweza kuanzishwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za wanyamapori.

6 HITIMISHO

Zoezi la kutenga na kuupandisha hadhi msitu wowote wa asili kuwa msitu wa hifadhi kwa mujibu wa sheria ya misitu na 14 ya mwaka 2002 ni mchakato. Ni mchakato kwa sababu hutanguzana na hatua kadha wa kadha ili ukamilike. Hali kadhalika zoezi la kuufanya msitu huria wa Tongwe kuwa msitu wa hifadhi wa Halmashuri ya Wilaya ya Mpanda ni mchakato wenye hatua nyingi. Kukamilika kwa hatua hii ya kufanya soroveya ya mipaka na kuibainisha kwa kushirikisha vijiji jirani kunatoa fursa ya kuingia hatua nyingine ndogo ya kufanya maamuzi ya dhati baada ya eneo halisi kufahamika. Hatua hii itatoa fursa kwa hatua nyingine kuu ya kufanya tathimini ya kiasi cha rasilimali zilizomo ndani ya msitu huo. Hatua hiyo inadhumuni la kupata mpango wa usimamizi wa msitu huo utakaoambatanishwa pamoja na andiko la kupeleka maombi ya Halmashauri yetu kwa Waziri wa Malisili na Utalii mwenye dhamana ya kuutangaza msitu huu kuwa msitu wa hifadhi. Taratibu hizi zote ni kwa mujibu wa Sheria ya misitu Na 14 ya mwaka 2002 kifungu cha 22 kifungu kidogo cha *1-4* na kifungu cha 23 kifungu kidogo cha *1-10*.

Nawasilisha kwa niaba ya Kikosi Kazi

Lucas Sotery Nyambala
Kiongozi wa Kikosi Kazi

VIAMBATA

Kiambata A: Barua ya Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Vikonge